

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

610

UALIMU

Muda: Saa 3

Jumanne, 7 Mei 2013 asubuhi

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na swali **moja (1)** kutoka katika kila sehemu B, C, D na E.
3. Sehemu A ina alama 40, sehemu B, C, D na E zina alama 15 kila moja.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Eleza matumizi manne ya Saikolojia ya Elimu kwa mwalimu.
2. Eleza kwa kifupi kampeni nne zinazohusishwa na harakati za uimarishaji wa Elimu ya Watu Wazima nchini Tanzania katika miaka ya 70.
3. Bainisha sababu nne za kutoa mitihani shuleni.
4. Orodhesha makundi manne yanayonufaika kutokana na tathmini na upimaji katika elimu. Andika kwa kifupi jinsi kila kikundi kinavyonufaika.
5. Bainisha mambo manne yanayopaswa kuzingatiwa wakati mwalimu anawasiliana na mwanafunzi kiziwi anapokuwa darasani.
6. Eleza kwa kifupi jinsi ambavyo urithi unaweza kuathiriwa na mazingira katika mchakato wa ukuaji wa mtoto.
7. Andika tofauti mbili kati ya upimaji na tathmini katika elimu.
8. Bainisha athari nne zinazoweza kutokea kutokana na mabadiliko ya mtaala ya mara kwa mara.
9. (a) Taja aina nne za viongozi.
(b) Dhana kuhusu kazi ya ualimu inayomchukulia mwalimu kama kiongozi ambaye ni kisima kikuu cha maarifa ni dhana iliyo dhaifu. Eleza udhaifu wa dhana hiyo.
10. Nyanja ya stadi imegawanyika katika ngazi mbalimbali. Eleza kwa kifupi ngazi nne zilizomo katika nyanja hii.

SEHEMU B: SAIKOLOJIA YA ELIMU (Alama 15)

Jibu swali **moja (1)** kutoka katika sehemu hii.

11. Watoto hujifunza vizuri kusoma, kuandika na kuhesabu katika umri kati ya miaka sita hadi saba. Kwa kutumia nadharia mojawapo ya kujifunza, eleza hoja sita za kuthibitisha kauli hiyo.
12. (a) Eleza kwa ufasaha matatizo matatu yanayohitaji ushauri nasaha shuleni.
(b) Eleza madhara matatu yanayoweza kujitokeza kwa mwanafunzi ikiwa matatizo yaliyoanishwa katika swali la 12 (a) hayakutatuliwa kwa wakati.

SEHEMU C: MITAALA NA UFUNDISHAJI (Alama 15)

Jibu swali **moja (1)** kutoka katika sehemu hii.

13. "Ni vigumu kwa mwalimu kuandaa azimio la kazi bila ya kuwa na muhtasari wa somo." Thibitisha kauli hii kwa kutumia hoja sita.
14. Umeteuliwa kuwa mwalimu mkuu wa shule ya msingi Kongowe. Baada ya kufika shuleni, unagundua kuwa wanafunzi wengi ni watoro. Bainisha sababu sita zinazoweza kuwa chanzo cha utoro huo. Pendekeza mbinu tatu zitakazosaidia kupunguza utoro shuleni.

SEHEMU D: UTAFITI WA KIELIMU, UPIMAJI NA TATHMINI (Alama 15)

Jibu swali **moja (1)** kutoka katika sehemu hii.

15. Mipango ya maendeleo ya elimu hufanikiwa kwa kutegemea matokeo sahihi ya tafiti za kielimu. Jadili kauli hii kwa kutumia hoja tano.
16. Eleza kwa ufasaha hatua tano muhimu zinazopaswa kufuatwa wakati wa kutathmini somo.

SEHEMU E: MISINGI YA ELIMU (Alama 15)

Jibu swali **moja (1)** kutoka katika sehemu hii.

17. Elimu ya kikoloni iliyotolewa katika vipindi mbalimbali hapa nchini ilikuwa na madhumuni yaliyofanana. Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kutumia hoja nne.
18. (a) Kwa kutumia hoja mbili jadili jinsi masuala mtambuka yanavyoweza kuingizwa kwenye mtaala shuleni.
(b) Jadili mbinu nne zinazofaa kutumiwa kuingiza masuala mtambuka katika masomo mbalimbali.